**** for the below sentences, please translate only the words in blue, leave the words in black in English**

**-----**

**Ikiwa kama ungetaka kuzungumuza na mtu fulani kabla hauja jiandikisha, tafadhali tuandikie barua pepe (email) kuhusu taarifa zinazo horodheshwa hapa chini kwa lugha ya Kiingereza. Hii itatusaidia kufahamu ikiwa kunahitajika kupata mkalimani katika utaratibu wa kuzungumza na wewe.**

Inahusu : *Interested in joining Survivor Alliance*

Ujumbe:

*Hi, my name is* [andika jina] *and I want to speak with someone about the Survivor Alliance. I speak* [andika lugha] *language.*

*I am able to speak the following dates and times:*
[weka tarehe na saa unayo weza kuzungumuza. Tujulishe njia tatu za uwezekano. Tafadhali tuambie unapatika kwenye eneo gani la wakati na kumbuka kuwa sisi tuko kwenye wakati wa UK - Uingereza]

**-----**

**** from here, please translate everything into Polish**

## KAZI

Kuunganisha na kuwatia nguvu walionusurika na utumwa na biashara ya wanadamu ulimwenguni kote

## SISI NI AKINA NANI NA KAZI GANI TUNAYO IFANYA ?

- Shirika la Walionusurika ni Muungano Usio wa Kiserikali (NGO) ambayo inaunganisha na kuwatia nguvu walionusurika  na utumwa na biashara ya wanadamu ulimwenguni kote.
- Tunaunda mtandao wa kimataifa wa viongozi miongoni mwa walionusurika ambao wanajihusisha na kazi ya kupambana na utumwa au wanaovutiwa na jambo hili ili kujihusisha.
- Tutasaidia maendeleo ya mitandao ya walionusurika, na tutaunganisha mitandao iliyopo kote ikiwapo kwenye jiji, kwenye jimbo na kwenye mataifa.
- Shirika la Walionusurika itaandaa Mkutano wa Dunia mnamo majira ya kiangazi 2019 inchini Uingereza. Hii itakuwa mkutano wa kwanza unao kusanya walionusurika na kuandaliwa wao walionusurika.
- Tunashirikiana pamoja na washirika wengine katika kazi ili kuhakikisha kuwa sauti za Walionusurika zinapewa nafasi ya mbele katikati juhudi zozote za kupambana na utumwa. Tutasaidia na kuwezesha ushiriki wa Walionusurika inapowezekana.
- Kujiandikisha katika shirika hili kunafanyika bila malipo yoyote na kwa mtu yeyote anaye jitambulisha kama mtu aliyenusurika toka utumwa au biashara ya wanadamu, na ambaye anakaa katika nchi yoyote ile.

## KUWA MWANAMEMBA

### Inamaanisha nini kujiunga na Shirika ya Walionusurika kama mwanamemba ?

● Kuwa sehemu ya mtandao wa kimataifa, na wakitaaluma wa Walionusurika na biashara ya wanadamu na utumwa.

● Kupokea kwa hiari mashauri kuhusu taarifa inayo eleza kuhusu maisha yako / kwenye taarifa inayo eleza kuhusu historia ya kuelimishwa kwako na ya uzoefu wako wa kikazi.

● Kupata bila malipo nafasi kufikia jamii iliyo kwenye mutandao wa internet ili kuhusiana na viongozi wengine miongoni mwa Walionusurika.

● Kuwa na uwezekano wa kuamua kuwa nafikiwa na jarida letu lifikalo kwa njia ya barua pepe na ambalo twalitumia kujulisha fursa zilizopo ili kutoa ushahuri ao kutoa uongozi.
● Kuhudhuria kwa hiari vikao vinavyo wakusanya Walionusurika wao kwa wao pekee.
● Kuboresha Sheria (Manifesto) ya Uanamamba na kutusaidia kutia nguvu mtandao wa kimataifa wa Walionusurika.

## Tangazo kuhusu hali ya Uanamemba

Tafadhali soma kila moja ya taarifa hizi kwa uangalifu. Tunawaomba wanamemba wote wanaotaka kuungana nasi kushikilia taarifa hizi kama mambo tunayo yazingatia kimusingi.

**Tunaamini kwamba utumwa na biashara ya wanadamu zinaingiliana na aina nyingi za unyanyasaji.** Hii inahusiana na mambo ya kabila, jinsia, kiwango cha mapato, vijikundi vya kijamii, dini, kuingiliana kimwili, utaifa, uwezo wa mwili na kiakili, na zaidi. Tunafahamu kwamba matokeo ya kule kufanywa mateka kisheria na ule utumwa wa watu wa Kiafrika bado yanaonekana. Tunaamini kuwa ni muhimu kushugulikia matokeo haya, pamoja na ubaguzi mkubwa, dhuluma, na ubaguzi wa rangi dhidi ya watu weusi.

Tunaamini kwamba ni lazima kwamba kupambana na utumwa na kupambana na kule kuwafanya wanadamu kuwa bihashara viwe ni pambano zidi ya ugandamizaji.

Lazima tuunge mkono #BlackLivesMatter, na harakati zinazo pambana na unyanyasaji dhidi ya wanawake, zile zinazo pambana kwa ajili ya haki za wafanyakazi, haki ya hali ya hewa, haki kwa kizazi cha Windrush, haki kwa jamii ya LGBTQ, haki za watu wa kiasili na za wahamiaji, haki za makundi ya watu ambao bado hakuna taarifa zilizo andikwa kuwahusu, haki za walemavu, na mambo kama na hayo.

**Tunajenga Imani yetu katika mazungumuzo ya kila mtu na mwengine, wala sio kuzungumuza kwa niaba ya kila mmoja.**
*Sisi sio "sauti ya wasio na sauti". Kila mmoja wetu ana sauti. Wengine hujieleza kwa njia ya kuongea na umma au kwa njia ya kuandika, wengine kupitia hatua za utndaji wa jamii, na*

*wengine kupitia njia za ubunifu kama sanaa au kupiga picha. Tunazungumza tokana na yale tulio yapitia na kuyaona na kwa njia hiyo tunatiana nguvu ili kusikilizwa.*

**Tunatambua kuwa mambo tulioyapitia ni ya pekee na tena yanatofautiana**
*Tunatambua kuwa ufafanuzi wa Umoja wa Mataifa kuhusu bihashara ya binadamu ni pana na inaonekana kuwa yale aliyo yapitia kila aliye nusurika hayata wakilisha aina zote na misukumo yote ya bihashara ya binadamu. Kwa hivyo, tunajitahidi kuungana ili kuelimishana kila mmoja juu ya utofauti katika tuliyo yapitia ili kuweza  kuunganisha kila fursa iliyopo na aliye nusurika ambaye fursa hiyo inaambatana naye hasa.*

**Tunaamini kuwa nguvu ya "sisi" ni kubwa kuliko nguvu ya "mimi".**
*Kutokana na kwamba kundi la walionusurika ni kubwa na tena watu waliomo wanazo tofauti kadha wa kadha, yawezekana kwamba si kila wakati ambapo tutakuwa na maoni yanayo ambatana. Walakini, tunapokubaliana, sauti ya pamoja ituruhusu kuweka shinikizo kwa wanao zitunga sheria, na kusimama pamoja dhidi ya ukosefu wa haki, na katika kukusanya rasilimali pamoja, na katika mengi zaidi.*

**Tutatanguliza afya yetu na ustawi wetu kwanza.**
*Tunatambua umuhimu wa kuongoza kwa njia ya kuonyesha mfano. Ili kuwa viongozi madhubuti, wanaharakati, washauri, na wanamemba wa jamii, tutatanguliza afya yetu na ustawi wetu kwanza.*

**Tutakuza mbinu ya kutia maanani vidonda vya moyoni (kiwewe).**
*Tunatambua kuwa matukio yanayo acha vidonda vya moyoni vinatokea hapa na pale kote ulimwenguni. Tokana na hilo, tunagundua kuwa mtu yeyote, sio tu walionusurika na bihashara ya binadamu, anaweza kuasirika kwa kubeba vidonda vya moyoni vinavyo dumu. Kwa hivyo, tutakuza mfumo wa kutia maanani vidonda vya moyoni katika kila mahusiano, ikiwemo hasa katika tukio lolote linalohusiana na mtu aliyenusurika toka biashara ya wanadamu.*

**Tutakuza umoja na kujilinda dhidi ya mgawanyiko.**
*Kutokana na kwamba kundi la walionusurika ni kubwa na tena watu waliomo wanazo tofauti kadha wa kadha, twaelewa kuwa hali za kuwa za watu na mitazamo inaweza kufikia kugongana. Zaidi ya yote, tutapata msingi unao tuunganisha katika kulenga kushugulikia unyanyasaji tulio wahi kuupitia zamani na katika kulenga kwetu pamoja kuzuia biashara ya wanadamu, kuwalinda walioasirika, na katika kuwatia nguvu walionusurika. Tunatarajia kila mtu kukuza umoja na kujilinda dhidi ya mgawanyiko.*

**Tunajitolea kufanya kazi kwa heshima katika kupitia changamoto na migogoro.**
*Tunaamini kuwa tofauti za mitazamo ni jambo la kawaida na huleta faida. Walakini, changamoto na migogoro inapotokea, tutajibu kitaalam na tutatafuta kuyatatua kwa njia ya*

*kiraia na yenye heshima. Hatutaendeleza utamaduni wa "kupiga kelele". Kunapo tokea kutokukubaliana, tunawahimiza walionusurika kuzungumza wao kwa wao na ana kwa ana. Ikiwa mzozo hauwezi kutatuliwa, tunatarajia pande zote kuendelea kuishi kwa njia ya kitaalam na yenye fadhili.*

**Tunatambua kuwa kila mtu ana jukumu muhimu katika harakati za kupambana na utumwa na kupambana na mitandao inayo wafanya wanadamu kuwa biashara.**
*Tunaamini kuwa, ikiwa wanataka, walionusurika wote wanaweza kuchukua jukumu katika harakati za kupambana na utumwa na kupambana na tabia ya bihashara ya wanadamu. Hakuna mashurti yoyote inayo hitajika ili kufanya hivyo na wala hakuhitajiki kwamba ifanyike hali umma ukitazama. Kila aliyenusurika yuko kwenye safari ya kipekee na lazima aamue mwenyewe jinsi, au ikiwa, anataka kuhusika.*

## Kinacho Hitajika kwa Mwanamemba

✔ Mimi najitambua kuwa mtu anayenusurika kwa biashara ya binadamu na / au utumwa.

***Tovuti*** :
[https://www.unodc.org/unodc/en/human-trafficker/what-is-human-trafficker.html?ref=menuside]

Bihashara ya Binadamu: "Kumufanya mtu kuwa kama bihashara" inamaanisha kuajiri, kusafirisha, kuhamisha, kubeba au kupokea watu, kwa njia ya vitisho au matumizi ya nguvu au aina zingine za kulazimisha, kutekwa nyara, udanganyifu, magendo, matumizi mabaya ya madaraka au ya hali ya unyonge au tena kutoa au kupokea malipo au faida za kufikia idhini ya mtu anayedhibiti mtu mwingine, kwa madhumuni ya unyonyaji. Unyonyaji utajumuisha, kwa kiwango cha chini, unyonyaji wa ukahaba wa wengine au aina zingine za unyanyasaji wa kijinsia, kazi ya kulazimishwa au huduma, utumwa au mazoea sawa na utumwa, kulazimishwa kufanya kazi au kuondolewa kwa viungo;

*Utumwa:* "Utumwa ni hali au mazingira ya mtu ambaye nguvu za haki ya kumilikiwa kwake zinatendwa juu yake kwa sehemu ao kwa jumla."

✔ Nina angalau umri wa miaka 18.

✔ Ninajiunga kama mtu binafsi na sio kama mwakilishi wa shirika.

✔ Niko tayari kujulisha jina langu la kwanza na la mwisho na anwani halali ya barua pepe.
✔ Ninaelewa kuwa Jumuhiya ya Walionusurika hautoi huduma za moja kwa moja kama makazi, tiba, au msaada wa kisheria lakini itatoa rufaa.

## Maswali yanayohusu Kujiandikisha kama Mwanamemba

Asante Kwa shauku yako ya kujiunga na Shirika ya Walionusurika! Kabla ya kujaza fomu hii, tunataka ujue kwamba habari maalum na ya kibinafsi unayoshiriki nasi itahifadhiwa siri isipokuwa utupe ruhusa ya kuishiriki.

Walakini, habari itaongezwa na kusambazwa bila majina kwa umma kwa kutumia taarifa kama vile: "25% ya washauri wa Shirika ya Walionusurika hutoka nchi X", au "57% ya washauri hutoa hotuba kuu".

Jina lako kamili ______________________ (inahitajika)

Anwani yako ya Barua pepe ___________________ (Inahitajika)

Je! Ni yapi ya maneno yafuatayo ambayo unatumia kuelezea uliyo wahi kuyapitia? (Inahitajika)

(Toa majibu kwa yote uonayo ilikuhusu)

Utumwa
Bihashara ya binadamu
Kulazimishwa kazi
Kazi ya dhamana
Utumwa wa majumbani
Uaskari wa watoto
Utumwa wa deni
Ndoa iliyolazimishwa
Bihashara ya ngono kwa Watoto (CSEC)
Bihashara ya ngono
Kunyanyaswa kwa bihashara ya wafanyikazi
Nyingine: __________________________________

Kwa sasa hivi naendelea kutoa huduma ya kusema, mafunzo, au ushauri katika uwanja wa kupambana na utumwa / mambo ya bihashara ya unyanyasaji wa binadamu. (Inahitajika kueleza)

Ndio

Hapana
Hapana, lakini nataka

Je! Wewe unaishi katika mji gani? (Hiari)

Unaishi katika nchi gani? (Inahitajika)

Tafadhali jibu kila sharti la kujiandikisha kama mwanamemba na ambalo linakuhusu. (INAHITAJIKA)

Nina umri wa miaka 18.

Ninajiunga na Jumuiya ya Walionusurika kama mtu na sio kama mwakilishi wa shirika.

Nimesoma Makubaliano ya yanayo hitajika kwa Uwanamemba.

Ninakubali kuruhusu wafanyakazi wa Shirika la Walionusurika (Survivor Alliance) waingilie uchunguzi kunihusu ikiwa wanahisi kuwa mimi sizingatii Makubaliano ya Uanamemba. Ninaelewa kuwa naweza kupoteza haki yangu ya kuwa mwanamemba kwa kukiuka Makubaliano ya uanamemba.

Ningependa kupokea mashauri ya bure kuhusu maelezo ya historia ya maisha yangu binafsi.
Ndio
Hapana

Napenda kupokea bila malipo ushauri kuhusu historia ya elimu na kazi nilizo wahi kuzifanya (CV).
Ndio
Hapana

Tutakuwa tukilituma jarida la kila mwezi na vilivyo jiri vya hivi karibuni na vilivyo vya muhimu toka kwa Jumuhia ya Walionusurika, pamoja na a) fursa za kushauriana na / au maendeleo ya wataalamu na b) rasilimali na harakati za kupambana na utumwa.
Je! Ungependa kupokea jarida hili? (Jibu linahitajika):

Ndio, tafadhali nitumieni jarida!
Hapana, sitaki kupokea jarida hili la vilivyo jiri la kila mwezi

Tafadhali toa majina na anuani ya email (barua pepe)/barua za mtu/watu waliokuelekeza kwa Survivor Alliance (Tafadhali kumbuka kuwa, tutawasiliana na anuani ya barua pepe uliyotoa ili kujuwa Habari na kupata mahakikisho kukuhusu. Hata ikiwa kama haukuelekezwa na mtu yeyote, bado tutakuwa tu na nia ya kukaribia. Tunaomba maelezo haya ili yatusaidie kuhusiana na usalama wa jamii ya Survival Alliance) :

............................................... .................................................

Tunataka kuwa na mazungumzo mafupi na ya kirafiki pamoja nawe kabla ya kukuongeza kama mwanachama. Tunahitaji mazungumuzo hayo ili tuweze kujifunza zaidi kukuhusu, kuhakikisha unajua tunachotoa, na pia ili kuweza kuambatanisha uso wa mt una jina lake. Tafadhali tuambie saa za eneo lako na upendekeze tarehe na nyakati chache unaoweza kuwa huru kwa mazungumzo kwa dakika 30 kwa kupitia Zoom. *

................................................ .....

Tafadhali tuambie ni vikundi au mashirika gani mengine ambayo umeunganishwa nayo. Unaweza kuongeza viungo vyovyote vya mahojiano na utuambie kazi ambayo umesha wahi kuifanya kama Kiongozi/Munusurika.

................................................ ........

Maswali mengine yoyote unayo kwetu? _______________________________________